REPUBLIC OF KENYA

COUNTY ASSEMBLY OF LAIKIPIA

THE HANSARD

Wednesday, 12th July, 2023

The House met at the Assembly Chambers at 9.00 a.m.

[The Speaker (Hon. Lantano Nabaala) in the Chair]

PRAYERS

QUORUM CALL

Speaker: Clerk, confirm whether we have quorum.

(Lack of quorum confirmed)

Speaker: I direct that the bell be rang for ten minutes.

(Quorum bell rang for two minutes)

Speaker: Having the quorum, I direct that the bell be stopped.

NOTICES OF MOTIONS

ESTABLISHMENT OF HUDUMA CENTRE IN RUMURUTI TOWN

Hon. Stephen Ndiritu: Thank you, Hon. Speaker, I am standing in on behalf of Hon. Caroline Kihika. I beg to move the notice of the following motion;

THAT, aware that Huduma Kenya Service Delivery Programme (HKSPD)is a Kenya Vision 2030 Flagship Project established vide the Kenya Gazette Notice No. 2177 on 4th April, 2014;

FURTHER aware that the Programme has the mandate to transform Public Service Delivery in order to ensure access to efficient, effective and citizen-centric services through One-Stop-Shop platforms;

CONCERNED that Rumuruti being the County Headquarters doesn't have a Huduma Centre; noting that the residents from the neighbouring town travels quite a distance in search of Government Services;

THIS House urges the County Government to liaise with the relevant Government Agencies to establish a Huduma Centre in Rumuruti Town. Thank you.

MOTION

ESTABLISHMENT OF HUDUMA CENTRE IN RUMURUTI TOWN

Hon. Stephen Ndiritu: Asante Bwana Spika. On behalf of Hon. Caroline Kihika, I beg to move the following motion;

THAT, aware that Huduma Kenya Service Delivery Programme (HKSPD)is a Kenya Vision 2030 Flagship Project established vide the Kenya Gazette Notice No. 2177 on 4th April, 2014;

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor*

FURTHER aware that the Programme has the mandate to transform Public Service Delivery in order to ensure access to efficient, effective and citizen-centric services through One-Stop-Shop platforms;

CONCERNED that Rumuruti being the County Headquarters doesn't have a Huduma Centre; noting that the residents from the neighbouring town travels quite a distance in search of Government Services;

THIS House urges the County Government to liaise with the relevant Government Agencies to establish a Huduma Centre in Rumuruti Town.

Thank you.

Bwana Spika, huu ni mswada ambao unauliza serikali kuu na ile ya ugatuzi kuungana ili kujenga Huduma Centre. Flagship Project Vision 2030 ambayo ilianzishwa na marehemu Rais Mwai Kibaki imezidi kuelekeza na kufanikisha mambo mengi nchini. Huduma Centre ni mahali ambapo mwananchi anaweza kupata huduma zozote kutoka Wizara tofauti katika jengo moja.

Nia kuu ya Mswada huu ni kuwasaidia watu wanaokaribia Rumuruti. Jiji la Rumuruti ndilo *Gazetted Headquarter* la Kaunti ya Laikipia. Hili ni jiji linalokua kwa haraka. Wananchi toka huko wanateseka sana kwa sababu wakihitaji msaada wa ofisi za serikali inawabidi kwenda Nanyuki, Nyahururu, Nakuru au Maralal. Huduma ikiwa Rumuruti, itaweza kusaidia wananchi wa Sosian, Marmanet, Mukogondo West, Salama, Segera, Kinamba na sehemu zingine nyingi za Kaunti yetu. Ni muhimu tuwe na Huduma Centre Rumuruti.

Juzi tumeona serikali ya Kaunti pamoja na serikali kuu wakifanya mpango wa kupeleka ofisi za mashamba Rumuruti. Tunataka huduma zingine zote zipelekwe pale. Zamani na sasa mtu anapohitaji sachi ya shamba, labda akuje Nanyuki. Haya ni mateso kwa wananchi. Sisi wakilishi wa Wadi ndio tumetumwa kuwatetea na kuzungumza kwa niaba yao. Tunaona ni vyema tuwe na Huduma Centre pale Rumuruti.

Mswada huu ulioletwa na Mheshmiwia Kihika ni wa kufaa sana. Hon. Umija anafahamu hivyo kwa sababu amefanya kazi na NGOs na anajua masaibu mengi kuhusu Rumuruti. Nafanya haya kumtayarisha ili akija kuaafiki Mswada huu ajue kwamba anauelewa zaidi.

Wanaotoka Rumuruti na kwingine kunakozunguka hapo, wanajua umuhimu wa Huduma Centre kujengwa Rumuruti. Tuko na Huduma Centre hapa Nanyuki na inawafaa sana wananchi wa Umande, Thingithu, Nanyuki na kwingine. Vitu kama *good conduct certificate*, kitambulisho na cheti cha KRA vitapatikana kwa urahisi sana kwenye Huduma Centre.

Kwa maoni yangu, Rumuruti ni jiji litakalo kuwa kubwa kushinda Naromoru, Chaka na town zingine baada ya miaka kama nne inayokuja. Ni tumaini letu kwamba baada ya miaka kumi, Rumuruti itakuwa kubwa kushinda Nanyuki na Nyahururu. Ni jiji ambalo huduma kwa mwananchi zitapatikana kwa haraka.

Huduma Centre ikijengwa Rumuruti, itasaidia wananchi wengi sana. Cheti cha Kuzaliwa itapatikana kwa urahisi. Baada ya kiangazi, baridi imeingia na unafahamu matokeo ya baridi nyingi ni watoto wengi kuzaliwa. Haya ni mambo yanayotusukuma kupata hio *Huduma Centre*.

Bwana Spika, nataka kumuita Mheshimiwa Umija ambaye anaelewa huu mswada na pia ni rafiki wa dhati wa Mheshimiwa Kihika ili tuweze kusaidia watu wa Rumuruti.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor*

Hon. Catherine Umija: Asante, Bwana Spika kwa kunipatia fursa ya kuongea kuhusu huu mswada. Ninaunga mkono huu mswada kuhakikisha ya kwamba tumepata huduma karibu na mwananchi. Mwananchi kulipa ushuru na kwa hivyo, inamaanisha ya kwamba ni lazima huduma iwe karibu na mwananchi. Inamaanisha ya kwamba zile huduma ambazo mwananchi anahitaji ni lazima ziwe karibu naye.

Nataka kushukuru Mheshimiwa Stephen kwa kufafanua umuhimu wa kuwa na huduma karibu na mwananchi. Hiyo ni kumaanisha ya kwamba wananchi hawataenda mbali kupata huduma. Watapata huduma karibu na pia kutakuwa na maendeleo kadhaa katika Mji wa Rumuruti.

Rumuruti ndio Mji Mkuu wa Kaunti ya Laikipia na lazima tufanye huo mji ukue na ndio tunaambia serikali iweze kuungana na Serikali Kuu ndio waweze kuhakikisha ya kwamba huduma zimefikia wananchi wote. Asante.

(Question proposed)

Hon. Simon Kanyutu: Thank you, Mr. Speaker. I stand to support the motion by the Hon. Kihika on Huduma Centre. Rumuruti, is the headquarters of this county and it is unfortunate that in the whole of Laikipia, we do not have a Huduma Centre. Whenever we require any services, we travel to Nyeri or Nanyuki. We were even thinking that we are a bit lucky because there is one that is being built at Makutano and we thought that that will be our nearest.

It is unfortunate because people from Olmoran travel all the way to Nyahururu and then to Olkalou because that is the nearest and because our road from Nanyuki to Rumuruti is very pathetic. I am wondering whether the government by 2030 will be able to see equal distribution of resources as it had been proposed. The people who distribute these projects do not try to check on the situation on the ground.

Now, I am lucky because instead of travelling to Nyeri, if the Makutano one would be initiated, that would be the easiest. When the National Government will be doing the distribution of resources, we need to see to fight for our people to get proper services.

Mr. Speaker, it is unfortunate because if you get somebody travelling from Survey and requires Huduma services, from Survey to Olmoran is quite a distance and then from Olmoran to Sipili to get a vehicle that will take him to Nyahururu. From Nyahururu again to either to Nyeri, Nanyuki, Olkalou or Nakuru. I am sure that the people from Laikipia West are really suffering. I am also concerned because it's a whole constituency with almost 150 registered voters. This is a requirement that should be done when the Huduma Centre distribution were being initiated.

I support and thank the Hon. Member for raising that concern. There is one Hon. Member who stated that Rumuruti is a small town that is growing but Rumuruti is a big town all the way from the colonial rule. That is where the word Rumuruti came from because it was known as a remote route towards Maralal.

We even had the judiciary by then in Rumuruti. As leaders, we are downgrading it and not prioritizing it for development. I am sure that very soon, even the Assembly will relocate to Rumuruti. So, as we seek for the Huduma Centre, even all the other government facilities ought to be in the county headquarters.

Hon. Catherine Nyokabi: Asante sana, Bwana Spika. Kwanza ni kushukuru Mheshimiwa Kihika na la pili nishukuru yule ambaye ameleta huu mswada kwa hili Bunge

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor*

kwa sababu ameelezea hadi tukaelewa kwa sababu huu mswada ulikuwa unatoka ndani ya roho yake. Ni kumaanisha ya kwamba walikuwa wameshirikiana na Kihika na kuona umuhimu wa kupeleka huduma katika Rumuruti. Niwashukuru kwa kuwa na ule utu na kujali wale watu wetu ambao wako mashinani na ambao walifanya tuwe mahali hapa.

La pili, nishukuru Maulana. Naona ya kwamba mnang'ang'ania huduma ipelekwe Rumuruti ambapo ni Mji mkuu wa Laikipia. Nashukuru Rais na Naibu wake kwa sababu hivi karibuni tutakuwa na Huduma Centre pale Ngobit. Ni kumaanisha ya kwamba wale viongozi ambao tuko nao tuko na utu na tuko hapa ili kuwakilisha wale watu ambao waliotuleta katika hili Bunge.

Kwa hivyo, mimi ningeomba ya kwamba watu wa Laikipia Magharibi wakisema ya kwamba serikali ishirikiane nao, pia viongozi wa Laikipia Magharibi washirikiane ndio Mbunge wao pia aweze kubisha milango katika Serikali Kuu ili hata wao waweze kupata Huduma Centre. Sasa hivi kwa sababu hawana na sioni kama itakuja hivi karibuni, tunawakaribisha pale Wadi ya Ngobit ili mtuletee kazi na biashara. Pia huko kwetu tuko na ploti mafuta mafuta ndio hata eneo la Ngobit likue. Asante.

Speaker: Thank you, Hon. Catherine. I wish to give the floor to Hon. Parleto Lekopien and maybe, you can let the House know of the original 1904 agreement that was signed in Rumuruti. Welcome.

Hon. Parleto Lekopien: Thank you, Mr. Speaker. On the point of the agreement, I don't have enough information but thank you. I am standing to support the motion and I am so impressed that this motion was read on behalf of Hon. Kihika by my good friend Hon. Kagondu coming from East, living around Nanyuki and getting all the services in Nanyuki. He is also very close to Nyeri despite of having a good road from Nanyuki to Nyeri. I am just impressed that he spoke from a willing heart that he wants the people from Rumuruti to benefit with services.

As I stand in support of the motion, my good friend Hon. Kanyutu just said that the people from Sosian, Olmoran, Salama and Rumuruti have suffered for a very long time. Even before we went for elections, all the services we needed to clear ourselves for elections, we had to travel all the way from Sosian and Rumuruti to Olkalou, Nanyuki or Nyeri. The accessibility of Nanyuki from Rumuruti is very pathetic. You have to go all round to Nyahururu and then to Olkalou.

We just want to compel the government to please support and ensure that we get all the necessary services in Rumuruti because it is growing. As we speak, Rumuruti is already a big town and we have got several services there like the court and the land registry. The only thing that is missing in the Laikipia County headquarters is the government services.

Before it was indicated as the county headquarters, I think that it could have been like yesterday that all the county services moved to Rumuruti. The buildings are ready and everything else and therefore, I think that it is just a matter of time and it should be very soon that all the services should be moved to Rumuruti.

On that point, as soon as we get all the services, we also need the Huduma services so that one will not need to leave his/her office to travel all the way to Nanyuki. You can just imagine if the Assembly moves to Rumuruti and you need the Huduma services, will you have to leave the session and come here? No. It is also very good for the people of Sosian that the services will be closer to them. Sometimes before Hon. Kihika thought of the motion, I was

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor*

thinking of moving the same that we need a Huduma Centre in Posta because that is the centre of Laikipia North.

As Hon. Nyokabi said, they already have Huduma Centre in Ngobit. I support the motion and I feel it could have come earlier so that the people of Sosian, Rumuruti and Olmoran can access and enjoy services equally as the people of Nanyuki. Thank you.

Hon. Salim Edung: Nashukuru Bwana Spika kwa nafasi hii. Kwanza ni pongezi kwa Mheshimiwa Kihika kwa kuleta mjadala huu kwenye Bunge hili kwa sababu imefungua watu wengi macho. Inamaanisha wale walikaa hasa Mheshimiwa Kihika na Umija wakaona nizuri watu wa Rumuruti wapate huduma. Kutoka mwaka wa 2013 ndio ugatuzi ulianza ambapo inasema lazima huduma zipatikane mashinani.

Nikiwa mwakilishi wa Segera naona kilomita 24 hadi Nanyuki. Nikiangalia ndugu yangu Mheshimiwa Lekopien na Kamara. Huduma ikiwa pale Rumuruti watapunguza nauli yao ya kukuja Nanyuki. Naunga mkono kwa asilimimia 100% kuwa huduma hii iwekwe Rumuruti ndio watu wasaidike.

Kazi yote ya serikali katika Bunge hili itahamishwa hadi Rumuruti. Kama hakuna kituo cha Huduma, watu wataendelea kwenda Nanyuki, Ngobit ama Nakuru na itakuwa changamoto. Mpangilio ya Kituo cha Huduma kipewe kipao mbele. Nashukuru hasa yule ameleta huu mjadala. Asante.

Hon. Anthony Theuri: Asante sana Bwana Spika. Sina mengi, kwanza ni kupongeza na kuunga mkono huu mjadala wa Mheshimiwa Kihika na vilevile Mheshimiwa Kagondu ambaye amekuwa mtumishi mzuri ama punda mwema ambaye husema, mzigo ifike punda ikufe. Lakini Mungu ni mzuri kwa sababu mzigo imefika na punda iko imara. Nimemuita hivyo kama mfano.

Ya pili, nashangaa. Naonea wenzangu huruma. Kamara, Salim, Gatati na Lekopien; hao wote kutoka mashariki. Kilio chao naelewa. Tumekuwa watu a kuongea kila asubuhi. Kutoka Rais wetu na naibu wake, Wabunge wajumbe na sasa wananchi wamefunzwa na kulia kilio bila machozi. Tunaongea maneno ya Rumuruti, tunataka Kituo cha Huduma kipelekwe Rumuruti. Kama Bunge, tumefanya nini kuhakikisha Rumuruti inaendelea? Mambo hugeuka. Jana nilikuwa Mwenyekiti, juzi Mheshimiwa Leila; mambo hugeuka lakini neno la Mungu haligeuki. Katika Mathayo, yesu aliambia watu mahali utajiri wako uko ndio roho yako iko hapo. Sisi Rumuruti iko kwa mdomo tu.

Juzi tulipitisha bajeti hapa. Ni nini ya Rumuruti ilikuwa pale? Sitaki kumpa changamoto Mheshimiwa wa Rumuruti sababu hayupo hapa. Nafahamu ana mambo anayoshughulikia na hivi karibuni atakuja. Nini tumeweka Rumuruti? Tunafahamu kuwa mahali utajiri wako uko, roho pia imo hapo. Miaka nenda miaka rudi tangu nikiwa kijana mdogo tunasema barabara ya kutoka Nanyuki kwenda Rumuruti itajengwa. Mwanangu yuko karibu kumaliza shule na bado haijajengwa.

Ina haja gani mimi kuja Bunge kila asubuhi kama shule? Mheshimiwa Gatati analeta mjadala wa Salama tunasoma na kwenda nyumbani. Mambo haya yanakera. Ikiwa tuna uhakika na haja na Rumuruti, basi tuanzeni kazi hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, zungumza na Mheshimiwa Leshuel ambaye ndiye anasimamia kamati ile na kazi ya ujenzi ianzwe. Tunapozungumza sasa hivi, uwanja wa Bunge wa Rumuruti hatujapanda hata maua. Gavana anaendeleza kazi vyema na nilipotembea huko juzi niliona ameanza kugawa maofisi. Kama tunataka kusaidiwa na kusaidika hasa sisi wachanga katika siasa, lazima tuanzeni kutimiza tunachozungumza hapa. Heri iwe kidogo lakini

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor*

tunatimiza. Kwa hayo, naunga mkono mswada huo. Tukimaliza hii, ningeomba tupewe *Spartial Planning* tuanzeni kazi pia.

Kwa vile Rumuruti iko Laikipia West, Mheshimiwa Wachira Karani naye aanzishe kutengeneza barabara. Hivi ndivyo tutajua na kuonyesha watu ya kwamba kazi inaendelea. Naketi sasa kwa vile naona Mheshimiwa Kanyutu hataki kuniombea niokoke. Nimemaliza, asante.

Speaker: Thank you Hon. Theuri. Today you have spoken golden words that apart from moving Motions, discussion and Debates, we should have actions following. Hon. Kanyutu.

Hon. Simon Kanyutu: I wanted a clarification on how do we implement? Our role here is to pass the law and there are people who are to implement. He is challenging on implementation. We pass the law and then those who should implement fail.

Speaker: Hon. Kanyutu please let the Deputy Speaker to respond.

Hon. Antony Theuri: Thank you, Mr. Speaker. I am conversant with the roles of the MPs, MCAs and Senators? What I am saying is that for us the MCAs, if we pass any law even if we are not the ones to implement, we should oversight. If the committee headed by Hon. Leshuel gives a road that will cross from here to the hospital and up to Tigithi ward and we pass it here, there is a committee that should follow up. Yes, we are not able to implement everything but we can oversight everything.

You can bring a Statement saying I said this and nothing happened. I have asked a question on what the Spatial Planning is waiting for. It is not a baby, let me not continue. Thank you.

Speaker: This was an indeed robust discussion. I know Hon. Stephen Ndiritu might be wanting to give a response. Let me give the floor to Hon. Benson.

Hon. Benson Kuria: Asante, Mheshimiwa Spika kwa kunikabidhi hii nafasi. Bila shaka, nimefurahia kwa sababu leo umevaa mavazi ambayo sijawahi kuona. Naona kuna mambo mazuri ambayo utatuelezea. Mheshimiwa Spika, naunga mswada huu mkono ambao umeletwa na mwenzangu mteule kwa Chama cha UDA, Mheshimiwa Caroline Kihika ambao pia umeweza kuletwa katika Bunge letu na Mheshimiwa Ndiritu ambaye pia amechaguliwa kwa chama cha UDA, Thingithu.

Huu ni mswada mzuri kwa sababu tukiangalia katika jimbo letu la Laikipia, watu wameweza kufunguka mawazo yao. Nikiangalia Vision 2030, inasema huduma bora kwangu na huduma bora kwa wananchi wa Laikipia. Hii inamaanisha huduma kwa mwananchi ambaye anatoa ushuru katika jimbo lake ama wadi yake. Ni vizuri awe akifikishiwa shughuli na kutendewa yale ambayo yanafaa.

Mheshimiwa Spika, najua ya kwamba huu muswada wa tuwe na huduma ndogo pale Rumuruti una nafasi kubwa sana ambayo Mheshimiwa Ndiritu na Mheshimiwa Anthony wameweza kutaja na kuguzia. Kuwe ya kwamba ili tuweze kufika Nanyuki ukiwa Kirimon, ukisafiri kwa bodaboda kutoka Rumuruti ni shilingi elfu tatu. Ukisafiri kutoka Maalam ambayo ni mpaka wa Baringo na Laikipia ili kufika Rumuruti utatumia elfu tatu na mia tano.

Kutoka hapo ili uweze kusafiri kutoka Rumuruti ili kupata huduma bora, itakuwa shilingi mia tano. Hii ni kumaanisha kwamba yule mwananchi ambaye anafaa kupata huduma bora hapati kwa sababu maisha ni magumu. Ukienda Marmanet kwa Wadi ya Mheshimiwa Kanyutu, akisafiri kwenda Nanyuki anatumia zaidi ya shilingi mia saba. Kwa hivyo, safari ya kwenda na kurudi inamgharimu shilingi elfu moja na mia nne.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor*

Atakula na atakunywa na kwa hivyo, huu mswada wa Mheshimiwa Caroline Kihika, Mheshimiwa Mteule kwa chama cha UDA ameafikiwa na Mheshimiwa wa Wadi ya Marmanet inaonyesha huduma bora kwa wanalaikipia inafaa katika vijiji zetu. Huduma Centre ikifika Rumuruti, Mheshimiwa wetu ambaye ni kijana kutoka Salama ambaye anacheza namba tisa nikicheza namba nane, najua tutafanya. Najua mambo yatakuwa sawa na wananchi wa Laikipia na wananchi wa Rumuruti, Ol Moran, Githiga, Marmanet na Sosian watakuwa wamejua ya kwamba Mungu amewaonekania.

Tusiwe tunanena kwa huu mswada ambao umeletwa na Mheshimiwa Ndiritu bali iwe ni kitu ambacho kitafanyika ili tuone ya kwamba sisi kama Waheshimiwa ambao wanatunga sheria katika jimbo letu wanafaulu. Mheshimiwa Spika, yangu ni hayo na ningetaka kusema ya kwamba kuna Liwaza ya 2030 ambayo ni *Vision 2030*. Nimeonyeshwa kwa roho kwamba Mheshimiwa Mugambi Gatati alikuwa anataka kuniuliza Liwaza ni nini. Asante, Mheshimiwa Spika.

Hon. Samuel Mugambi: Thank you, Hon. Speaker for giving me this chance. I am standing in support of the good motion. It is good I speak so that it goes on record since Rumuruti is neighbouring Salama with One Kilometre. I thank the mover of this motion, Hon. Kihika and the Member who presented the motion here. I also want to thank my brother Hon. Kamara for those good sentiments he has echoed in this House. Indeed, Huduma Centre is necessary in our county.

For the record, we have approximately 45 Huduma Centres in Kenya. In our county, we have one working in Nanyuki and another one is coming to Makutano. If it goes to Rumuruti, it will be good. Hon. Speaker, I recommend what the Deputy Speaker said here. There are other functions that we need to implement as a County Government so as to benefit our headquarters.

Recently, I attended a seminar at Rumuruti that was being carried by the World Bank. I run important things that the County Government of Laikipia is lacking and we are missing a lot of funding from the World Bank. Hon. Speaker, one is the World Bank is claiming that the County Government of Laikipia have not fully implemented the Rumuruti Municipality. By that, we are missing a lot of funding.

I want to say what the Deputy Speaker was saying here because an Englishman said what is good for the goose is good for the gander. That we need these policies and the projects that are entitled to the County Government need to be implemented then we start petitioning the National Government to bring their services like Huduma Centres. Hon. Speaker, in Laikipia County there is no functional municipality.

Rumuruti is the oldest but it is not functional. We only acquired the offices five months ago and if you go to the County Government Act, how a municipality should work is a municipality should have all devolved functions of the municipality. That is a requirement by the World Bank to get the grants. Other Counties like Kisii have already started receiving the grants. Even if we are passing laws, it is always good to pressure the Executive to pressure the relevant authorities to make all these headquarter functions to be fully devolved.

Thank you, Hon. Speaker, for giving me this chance. I have heard Hon. Kamara saying that there is something I am playing number nine and I do not know what he is insinuating but I thank him for the good comments. Thank you, Hon. Speaker.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor*

Speaker: Thank you, Hon. Mugambi Gatati. If there are no members who would like to contribute to the motion, I am grateful that all the Members seem to be affirmative on this motion. Without much ado, I will ask the mover of the motion to reply.

Hon. Stephen Ndiritu: Asante, Mheshimiwa Spika. Nataka kushukuru Waheshimiwa kwa kutoa maoni yao na kuchangia kwa huu mswada. Tunauliza Serikali ya Kaunti Pamoja na Serikali Kuu kushirikiana ili tuweze kuwa na Huduma Centre. Bwana Spika, kama mwenyekiti umesikia yale ambayo waliochaguliwa na wananchi. Ni muhimu kuwa na Huduma Centre katika Rumuruti ili tuweze kurahisishia wananchi wetu ili waweze kupata huduma kwa karibu.

Kama vile umesikia Mheshimiwa kutoka Sosian akisema wanaumia wakitoka mbali na pesa ambazo wanatumia. Unakuta wananchi wanatumia pesa nyingi ili kupata huduma lakini tukiwaletea, itakuwa inawasaidia sana. Vilevile ningependa kumweleza ndugu yangu hapa hata kama ametoka ya kwamba sisi kama Waheshimiwa, kazi yetu ni kuongea na kusema kwa sababu ndio maana tulichaguliwa kuongea kile ambacho kitafanyika leo na miaka kumi ijayo na miaka ingine.

Kwa hivyo Bwana Spika, nitaeleza ndugu yangu asikufe moyo hata kama tunasema mambo na haifanyiki. Kusema ni tofauti na kutenda. Kutenda ni lazima uweke pesa na kama hauna pesa, hilo jambo halitafanyika. Wakati tunaongea kuhusu Huduma Centre ni kuomba Serikali Kuu iungane na Serikali ya Kaunti. Mjadala umesema, *"we want the County Government and the National Government to liaise".*

Tunawaomba lakini sio kuwaambia wajenge Huduma Centre. Wanaweza kuwa hawana fedha kwa sasa lakini tunawaeleza wafanye. Singetaka kesho nikitoka hapa nikutane na Mheshimiwa Theuri akiuliza iko wapi. Haitawezekana, kwa hivyo huu ni mpango na hiyo ni kazi yetu. Kuna miradi ambayo huwa tunasema, kwa mfano mimi nitasema ninataka kitu fulani Thingithu. Nasema tu ili iwekwe kwa kumbukumbu na wakati pesa zitapatikana lifanyike.

Ni vizuri tunapoongea na kuuliza vile miradi inafanyika ili tuweze kuelewa ya kwamba tutakapokuja hapa ndio tutaweka pesa. Vilevile Bwana Spika, tunaposema kuenda Rumuruti, Mheshimiwa Theuri ameuliza swali muhimu sana kwamba sisi kama Bunge, tumefanya nini kuhakikisha Rumuruti imekua? Sisi tuko na mkono wa kufanya Rumuruti na Kaunti kwa jumla iendelee.

Tuko na shamba ya Bunge la Kaunti. Hata kama hatujajenga basi tupande maua na tuweke ua ili tuonyeshe tuko na nia njema. Vilevile Bwana Spika, tuko na Ukumbi ambayo iko Nyahururu na tukiwa Nyahururu, tuko karibu na Rumuruti. Tukiwa hapo, kuteremka ni rahisi na kwa hivyo Ukumbi ambayo tuko nayo hata kama ni wiki ijayo, haitagharimu pesa nyingi tunaweza kuchanga na Mheshimiwa Theuri hata kama yeye ni *hustler*. Tutachanga ili chumba kisafishwe ili tukafanye kazi Nyahururu.

Hata sisi tunaweza furahia tukitoka hapo twende Nyahururu. Vilevile, Mheshimiwa Kanyutu anaweza furahia sana kwa sababu tumekaribia kwake. Kila siku atakuwa akija Bunge na kurudi kulala kwake. Leo amekuja Bungeni na sijui atalala wapi, lakini Mungu atamsaidia. Atajivinjari hapa na pale na mambo hayatakuwa mabaya. Hata sisi tunataka hivyo, wakati mwingine tukitoka tunaenda kujivinjari huko kidogo na unaelewa kuwa sina nia mbaya ninaposema hivyo.

Vilevile, namshukuru Mheshimiwa Nyokabi kwa kusema kuwa mimi na Mheshimiwa Kihika ni marafiki. Kwa kweli, sisi ni marafiki na ndio maana nimeuleta huu mswada, lakini urafiki wetu haujavuka hio ng'ambo anayotaka kumaanisha. Wetu ni ule urafiki wa kuonana

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor*

na kusaidiana, hatujafika mahali ambapo yeye alidhani. Ila ikija, yote ni ya Mungu. Nani kama sisi? Ya Mungu ni mengi na ya kuku ni mayai.

Kwa hivyo, mimi ningetaka tuwe na umoja na tusaidiane. Kama Mheshimiwa Umija hayuko hapa, ninamsaidia kwa sababu tuko hapa kufanyia wananchi kazi. Kama Mheshimiwa Kamara hayuko ninamsaidia, naye akiona mimi sijafika kwa sababu ya mambo tofauti tofauti, ananisimamia na kuwasimamia watu wa Thingithu hadi nitakapokuja.

Bwana Spika, nataka kuchukua hii nafasi kukushukuru wewe pia kwa vile umetuongoza Bungeni tangu tulipoingia hapa. Umekuwa Spika mwenye hekima anayeelewa mambo kwa haraka na ambaye leo amevaa nguo nyingine mpya ambayo hatujawahi kuona. Tunashukuru kwa hayo mambo na tunaona kwa kweli tunasonga mbele. Kwa hayo machache, nawashukuru Wajumbe na kuwaomba tuupitishe huu mswada ili serikali iweze kuongea na ile nyingine ndiposa wananchi wa Rumuruti wapate maendeleo katika sehemu yao. Asante.

Speaker: Thank you, Hon. Stephen. Before we rise, I know that we have been away on recess but I want to remind us of a few things that we need to observe while in here. I would like to refer all Members to Standing Order No. 74. Allow me to read it:

1) *All proceedings of the Assembly shall be conducted in Kiswahili, English or in Kenyan Sig Language.*

2) *A Member who begins a speech in any of the languages provided for under paragraph (1) shall continue in the same language until the conclusion of the Member's speech.*

I realized a few of our Members from the recess have interacted with citizens and communicated in multiple languages. I remind all Members that in the next sessions let us observe Standing Order No. 74. Thank you.

(Question put and agreed to)

ADJOURNMENT

Speaker: The sittings of this House now stand adjourned until later today, Wednesday 12th July, 2023 at 2.30 p.m.

The House rose at 9.54 a.m.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor*